
# Taarifa Njema katika Maendeleo ya Umwagiliaji



**Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japani**
**Ofisi ya Tanzania**
**Disemba 2020**

# Utangulizi

***Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japani (JICA) limekuwa mshirika wa maendeleo kwa Tanzania tangu 1962.***




Skimu ya umwagiliaji ya Lower Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro

## *Nchini Tanzania, umwagiliaji umeongezeka kutoka hekta 274,000 mwaka 2008 hadi hekta 475,000 mwaka 2017.*


Moja ya mchango mkubwa wa JICA katika sekta ya kilimo ni katika kilimo cha umwagiliaji na maendeleo ya sekta ya mpunga. Ushirikiano wa JICA umeanza mnamo mwaka 1974 kupitia mradi wa "Mpango wa Maendeleo Jumuishi wa Mkoa wa Kilimanjaro"

Tangu wakati huo, JICA imejishughulisha na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika Mpango wa Umwagiliaji wa Lower Moshi (1984), Mpango wa Umwagiliaji wa Ndungu (1987), na Mpango wa Umwagiliaji wa Mwega (2000). Halafu, JICA ilisaidia kuandaa Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Umwagiliaji mnamo 2002 na kisha kurekebishwa mnamo 2018.

Baada ya kuandaa NIMP 2002, mfululizo wa ushirikiano wa kitaalam umekuwa ukitekelezwa ili kusaidia uboreshaji wa uwezo wa kuendeleza umwagiliaji, pamoja na ukuzaji wa uwezo wa wahandisi wa umwagiliaji na maafisa wa umwagiliaji kwa kuwapatia mafunzo ya kiufundi.




.




Ramani ya-Skimu za umwagiliaji zilizofadhiliwa na mradi (Doti zinaonyesha maeneo hayo).
)

Mradi wa mkopo unaoitwa Mradi wa kuendeleza skimu za Umwagiliaji (SSIDP) ulikarabati au kujenga miradi midogo ya umwagiliaji zaidi ya 100 yenye (uwezo wa umwagiliaji chini ya hekta 500) kote Tanzania (tafadhali angalia ramani.

Wahandisi wa umwagiliaji , maafisa wa halmashauri pamoja na wakulima wa vyama vya umwagiliaji wameshiriki katika mafunzo mbalimbali ya vitendo ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya mpango wa umwagiliaji, kama vile uundaji na utekelezaji (F&I) na uendeshaji na matengenezo (O&M) ya skimu za umwagiliaji.




Banio - lilifadhiliwa na mradi wa umwagiliaji

## Miradi wa kujenga uwezo

**TANCAID (2007.1-2010.1):**
**Kuandaa CGL (Mwongozo kabambe wa Maendeleo ya Umwagiliaji), na kuusambaza kwa serikali kuu.**
**TANCAID (2010.12-2014.6):**
**Kusambaza CGL kwa nchi nzima. Mafunzo yalifanywa kwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa (LGA) 132.**
**TANCAID2 (2015.8-2020.8):**
**Kukuza matumizi endelevu ya CGL.**
**1. Utekelezaji Kwa vitendo wa CGL chini ya SSIDP.**
**2. Kuboresha usimamizi wa miradi yote ya maendeleo ya umwagiliaji kupitia kuanzishwa kwa mfumo wa ufuatiliaji / utoaji taarifa**
**3. Kuboresha uwezo wa utekelezaji wa Halmashauri.**

Pamoja na maendeleo ya miundombinu ya umwagiliaji, JICA pia imesaidia kujenga uwezo juu ya kilimo cha mpunga kote nchini. Sasa, Tanzania inajitosheleza kwa uzalishaji wa mpunga

### Uzalishaji wa Mpunga na Eneo linalozalishwa




# Shughuli chini ya CGL

*Uundaji na Utekelezaji wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji*









Manual for Standard Design of Irrigation Canal

(Ver.1.1)

for

Technical Cooperation for Capacity Development
for the Promotion of Irrigation Scheme Development
under the District Agriculture Development Plans (DADPs)

Sept. 2017

National Irrigation Commission, Ministry of Water and Irrigation (MoWI)

*Ukarabati wa skimu ya umwagiliaji ya Ulyanyama, mkoa wa Tabora*

**Kabla ya ukarabati**



**Baada ya ukarabati**






*Mafunzo ya ukarabati shirikishi*

*Uendeshaji na Matengenezo Shirikishi*



**Uundaji na Utekelezaji wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji**

**Idadi ya washiriki wa mafunzo kupitia TANCAID2**

**Wahandisi wa Umwagiliaji na maafisa: 3,000**

**Maafisa wa Serikali za Mitaa: 3,400**

**Vyama vya  Wakulima wa Umwagiliaji: 9,300**

## Bwana. Rajabu Juma Chejo

***"Kilimo cha umwagiliaji ni cha kuaminika kuliko kilimo cha kutegemea mvua. Kilimo ni Maisha yangu"***





Baada ya kuhudhuria mafunzo, niliwahimiza wakulima wengine, haswa wakulima wadogo, ni kiasi gani uzalishaji wa kilimo unanufaisha na kuweka umuhimu wa utendaji kazi, utunzaji wa skimu yetu ya umwagiliaji kwa bidii.

Mbali na kuchangia ada ya usimamizi wa umwagiliaji, kila wakati mimi hushiriki katika shughuli za uboreshaji wa skimu ya umwagiliaji. Matokeo ya kufanya bajeti ya kifamilia, pia faida ya uzalishaji wa mpunga niliwekeza katika kununua mashine mbili za kushona kwa ajili ya mke wangu ili kuongeza vyanzo vya mapato. Sasa mke wangu anafanya biashara ya ushonaji nyumbani.

Hatua inayofuata ni kuanza biashara ya kuongeza thamani ya mchele.

**Bi. Tatu Abdallah Rwambo**

***"Ninashiriki na wakulima wengine waliohamasishwa pamoja na wale walio nje ya mpango huu maarifa niliyopata kutoka mpango wa mafunzo ya Uendeshaji na Matengenezo ya kilimo cha umwagiliaji."***



Uzalishaji wa mpunga uliongezeka kutoka tani 5.6/ha hadi tani 6.4/ha kutoka kwa kutumia umwagiliaji wa uhakika. .Upatikanaji wa maji umeongezeka kwa sababu kamati ya usambazaji maji hufanya kazi vizuri. Ukusanyaji wa ada ya umwagiliaji umeboreshwa pia. Kabla ya mafunzo, tulilipa ada ya huduma kwa viongozi wa kamati ya umwagiliaji. Baada ya mafunzo, wanachama hulipa kupitia akaunti ya benki na kuwasilisha hati ya malipo kwa mweka hazina. Uwazi huo ulioboreshwa ulisaidia kupunguza upotezaji na matumizi mabaya ya fedha.

## Bi. Tatu Mrisho Mbogo

***"Niliweza kulipa ada ya masomo ya Chuo Kikuu ya mtoto wangu. Nilianzisha duka dogo na kununua viwanja baada ya kufanya kilimo cha umwagiliaji. "***

Kati ya Disemba na Mei, mimi hulima mpunga kwa kutegemea mvua na nyongeza kwa umwagiliaji, na mahindi kwa mvua. Kawaida mimi hupanda mpunga tena mnamo Julai, na huvuna mnamo Novemba. Msimu huu nimetegemea umwagiliaji tu.

Hapo zamani hakukua na mipango ya awali ya kugawana maji ya umwagiliaji. Baada ya mpango wa uendeshaji na usimamizi, ugawaji uliopangwa wa maji ulipunguza migogoro kati ya wakulima.



Sasa wanachama wote wanapata maji kulingana na ratiba ya usambazaji wa maji ya umwagiliaji.



**Bwana. Simoni Elieza Kalosa**

***"Mnamo mwaka wa 2017 nilipata mazao ya mpunga ya tani7.5/ha baada ya mafunzo. Mwaka 2015 mavuno yalikuwa tani 1.7/ ha "***



Mimi hulima mpunga katika skimu ya umwagiliaji wakati wa mvua na kwa nyongeza ya umwagiliaji. Wakati wa kiangazi, mimi hulima mpunga kwa umwagiliaji. Mahindi na njugumawe huzalishwa kwa kutegemea mvua kwenye maeneo ya uwanda wa juu.



Ninaelewa tunachotakiwa kufanya katika usimamizi wa skimu ya umwagiliaji. Pamoja na familia yangu, nilishiriki katika kazi ya kusafisha mfereji na matengenezo.

Kuongezeka uwazi wa matumizi ya ada iliyokusanywa ya umwagiliaji kulituchochea kuchangia usimamizi wa skimu ya umwagiliaji. Baada ya mafunzo, malipo ya ada ya huduma ya umwagiliaji yamekua rahisi zaidi na hulipwa kwa urahisi kuliko hapo awali. Sasa, wanachama wanachangia mfuko mmoja (95kg) wa mpunga kwa ekari moja kwa ada ya maji na ada ya uanachama kwaajili ya usimamizi wa umwagiliaji.

## Bi. Amasidze Kosamu Kadwame

*"Nilikuwa nikichota maji kwa kutumia ndoo kumwagilia mazao. Sasa ninatumia maji tiririka kutoka kwenye mfereji wa umwagiliaji."*

Ninapanda mahindi mara mbili kwa mwaka kwa umwagiliaji na maharagwe kutegemea mvua. Mavuno ya mahindi na maharagwe yameongezeka hadi tani 7.5t/ ha kutoka tani 2.5/ ha na hadi tani 1/ ha kutoka tani 0.5/ha, tangu ujenzi wa skimu ya umwagiliaji.

Nimejenga nyumba mpya yenye vyumba vinne vya kulala na kuweka umeme, nimenunua kuku 20 wa kufugwa na nililipia ada ya shule kwa watoto wangu hadi kidato cha nne cha sekondari.





## Bwana. Kasala Nasani Mihambo

***"Baada ya mafunzo, ninaelewa kuwa lazima nilipe ada ya huduma ya umwagiliaji ili niwe na uhakika wa maji ya umwagiliaji kwenye shamba langu. Tunatumia ada iliyokusanywa ya huduma kwa uendeshaji na utunzaji wa skimu ya umwagiliaji. "***



Niliboresha kilimo changu baada ya mafunzo juu ya usimamizi wa skimu ya Umwagiliaji. Nilifundisha kile nilichojifunza, kama faida ya uendeshaji & matengenezo, upangaji wa usambazaji wa maji kwa uboreshaji wa upatikanaji wa maji shambani na matokeo yake ya mavuno bora ya mazao.

Baada ya mafunzo, nilielewa kiwango sahihi cha maji ninachohitaji kwa zao hilo. Kabla nilikuwa nikitumia maji mengi kukuza mpunga. Sasa, kila mkulima anapata sehemu yake ya maji. Tunafanya mzunguko wa maji ya umwagiliaji ili kuruhusu kila mkulima kupata maji ya umwagiliaji sawa. Mfumo wa kugawana maji ni mzuri kwa wakulima kwani hauhitaji mkulima kutumia muda mrefu kutafuta maji, kwani maji husambazwa na bwana maji. Mfumo huu umepunguza migogoro juu ya matumizi ya maji na upatikanaji wake ni rahisi sana sasa.

Ninalipa ada ya huduma ya umwagiliaji kwa kiwango cha 5% ya mavuno ya wastani kwa ekari moja kulingana na mwongozo kabambe wa umwagiliaji. Mimi pia hushiriki katika mikutano ya vyama vya wakulima wa Umwagiliaji ili kuchangia maamuzi ya shughuli zinazohusiana na vyama vya wakulima wamwagiliaji. Tunatumia ada iliyokusanywa ya huduma kwa uendeshaji na matengenezo ya skimu ya umwagiliaji, pamoja na malipo kwa waajiriwa wa kawaida kwa kusafisha au kutengeneza mifereji na malipo mengine ili kudumisha kituo hicho.

Uzalishaji wa mpunga uliongezeka na nililipa ada ya shule kwa watoto wangu na kununua ng'ombe, kuku, pikipiki na kujenga nyumba nzuri kwa familia yangu.

**Mtu yeyote anaweza kuwa mkulima wa mfano!Tuchukue hatua kwa kushirikiana na wale wakulima waliofanikiwa ili kupata faida ya muda mrefu. Msaada wa kiufundi wa umwagiliaji unapatikana katika ofisi za serikali za mitaa au katika ofisi za tume ya umwagiliaji.**



**Bi. Fransisca Maulid Hongole, Skimu ya Mkombilenga , mkoani Iringa**
***"Sasa mavuno kutoka kwenye shamba la umwagiliaji yameongezeka na nimefanikiwa kununua trekta la mkono."***


## JICA Tanzania Office

3rd Floor, ABSA House 1008/1 Ohio Street, Dar es Salaam, TANZANIA
(P.O.Box 9450, Dar es Salaam, TANZANIA)
Tel : +255- 22- 2113727 - 2113730
Fax : +255- 22- 2112976
https://www.jica.go.jp/tanzania/english/index.html


Picha katika kurasa ya mbele: Bwana. Joseph Kizwalo Simon, skimu ya Nyida, Mkoa wa Shinyanga